# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

# BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO NGAZI YA 1

# NJOMBE RVTSC - 2025

Simu: 0738679333

P.O. Box 698, Njombe
njombervtsc@veta.go.tz
www.veta.go.tz

Nukushi:

Kumb. Na;

29/11/2024

---

Ndugu

………………………………………………………..

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NGAZI YA 1 CHUO CHA NJOMBE RVTSC MWAKA 2025

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika

   Fani ya 'ELECTRICAL INSTALLATION'

   Katika ngazi ya 1 (Level 1) - **Bweni (Boarding)**
2. Mafunzo yatachukua muda wa Miaka miwili (2)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 13/01/2025
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. **Fedha ikishalipwa hairudishwi**. Fedha za tahadhari (caution Money) hazitarudishwa badala yake zitatumika kwa ukarabati wa miundombinu ya chuo pale mwanafunzi anapo hitimu
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

Wilfred Mwatulo
MKUU WA CHUO

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA MKOA WA NJOMBE**

**MAELEZO MUHIMU YA KUJIUNGA KWA MWANACHUO WA NGAZI YA 1 – MWAKA 2025 (*MAELEZO HAYA YASOMWE KWA UMAKINI NA MWOMBAJI NA MZAZI/MLEZI WA MWANACHUO)***

## A: UTANGULIZI

- Mwanachuo azingatieni kufika siku ya tarehe **13/11/2025** kabla ya **saa 12:00 jioni**. Hatutapokea mwanachuo siku zisizokuwa za kazi na hupaswi kufika kabla ya tarehe ya kufungua chuo.

- **TAARIFA ZA CHUO**
  - **MAHALI:** Chuo kipo Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Ludewa, Kata ya Lugarawa katika Kijiji cha SHAURIMOYO
  - **NAMNA YA KUFIKA CHUONI:** Ukitokea Njombe Mjini unapanda basi la MKOMBOZI au MBWENI kwa nauli ya Tsh. 10,000/= hadi SHAURIMOYO eneo kilipo chuo.

## B: ADA NA MICHANGO NA NAMNA YA KUFANYA MALIPO KWA MWAKA

Kwa mwaka mzima ambao una mihula miwili, mwanafunzi wa bweni anatakiwa kulipa jumla ya Tsh. 270,000/=, na mwanafunzi wa kutwa anatakiwa kulipa jumla ya Tsh. 210,000/= kwa mchanganuo unaooneka katika jedwali hapo chini:

| AINA YA MALIPO | MUHULA WA KWANZA (JANUARI HADI JUNI 2025) | | MUHULA WA PILI (JULAI HADI DISEMBA 2025) | |
|---|---|---|---|---|
| | BWENI | KUTWA | BWENI | KUTWA |
| Ada ya mafunzo | 60,000 | 30,000 | 60,000 | 30,000 |
| Tahadhari | 30,000 | 30,000 | - | - |
| Michezo | 25,000 | 25,000 | - | - |
| Fulana (T-shirt) | 20,000 | 20,000 | - | - |
| Nembo ya VETA | 5,000 | 5,000 | - | - |
| Kitambulisho | 5,000 | 5,000 | - | - |
| Mahafali | 10,000 | 10,000 | - | - |
| Ada ya mtihani wa taifa | - | - | 25,000 | 25,000 |
| Ziara ya mafunzo (Study tour) | - | - | 30,000 | 30,000 |
| JUMLA | **155,000** | **125,000** | **115,000** | **85,000** |

**ZINGATIA:**

1. Fedha za ada na michango iliyoainishwa kwenye jedwali hapo juu italipwa kwa ‘control number’ ambayo itatolewa chuoni kabla ya mwanachuo kuanza masomo. Baada ya kulipa fedha **mwanachuo aje na risiti ya malipo iliyo andikwa jina lake ili apokelewe tayari kwa kuanza masomo.** Hatupokei fedha taslimu.

2. Mwanafunzi hatapokelewa kama hajalipa ada na mahitaji mengine yaliyoainishwa kwenye fomu hii kwa muhula husika. Ukifanya makosa wakati wa malipo, pesa iliyolipwa hairudishwi. **Malipo yote ya muhula husika yanalipwa kwa mkupuo mmoja (Hatupokei malipo nusu nusu)**

3. Kama utahitaji ufafanuzi wa jambo lolote lililo kwenye fomu hii wasiliana na Mratibu wa mafunzo kwa namba 0753469298.

**C: BIMA YA AFYA NA HUDUMA ZA MATIBABU KWA MWAKA**

Bima ya afya ni hitaji la lazima kwa kila mwanafunzi. Kwa asiye na kadi ya Bima ya afya (NHIF) aje na fedha taslimu **Tsh 50,400**/=. Mwanafunzi akifika chuoni atapewa 'control number' ya kufanya malipo ya Bima ya afya. Kadi hii itakuwezesha kupata huduma popote Tanzania, na pia ina wigo mpana wa matibabu kwa kuwa huduma zake zinapatikana kirahisi na kwenye vituo vingi vya afya.

Kwa yule aliye na kadi ya Bima ya afya, ahakikishe kadi yake haijaisha/kukaribia kuisha muda wake wa matumizi na atahitajika kuwasilisha kwa Msajili wa Chuo ili ihakikiwe (kadi ya Bima inayokubalika ni ya NHIF pekee).

**D: SARE ZA CHUO NA MAHITAJI MENGINE YA MWANACHUO**

1. Suruali 2 na Ovaroli au Ovakoti 1 vitapatikana kwa fundi Yusuph Kyando aliyetafutwa na chuo ili kuepusha kutofautiana kwa vitambaa endapo kila mwanachuo angeshona kwa fundi wake. Hivyo mwanachuo haruhusiwi kushona kwa fundi mwingine zaidi ya huyu, na mwanachuo anatakiwa kufika na fedha tasirimu na atamkabidhi fundi kwa mchanganuo ulivyoainishwa katika jedwali hapo chini:-

| Na. | SARE | IDADI | GHARAMA |
|---|---|---|---|
| 1 | Suruali rangi ya bluu | 2 | 40,000 |
| 2 | Ovaroli/ Ovakoti (bluu) | 1 | 40,000 |
| | **JUMLA** | | **80,000** |

2. Vifaa vifuatavyo utatakiwa kununua na kuja navyo wakati wa kuripoti kwa ajili ya matumizi yako ukiwa chuoni:-

| **Na.** | **MAHITAJI** | **IDADI** |
|---|---|---|
| 1 | Shati nyeupe ya tetron (mikono mirefu) | 2 |
| 2 | Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba(visigino vifupi) | Jozi 1 |
| 3 | Daftari kubwa (3 Quire) | |
| 4 | Ream ya karatasi (A4) | 1 |
| 5 | Sweta rangi ya bluu | 1 |
| 6 | Godoro futi 2.5 x 6, unene inch 3 **(Kwa mwanafunzi wa bweni)** | 1 |
| 7 | Mathematical set | 1 |
| 8 | Ndoo ndogo **(Kwa mwanafunzi wa bweni)** | 2 |
| 9 | Shuka **(Kwa mwanafunzi wa bweni)** | 2 |
| 10 | Safety boot nyeusi **(Kwa mwanafunzi wa fani ya Umeme, Uashi, na Bomba)** | Jozi 1 |
| 11 | Fyekeo kwa mwanafunzi wa kike<br>Jembe kwa mwanafunzi wa kiume | 1 |
| 12 | Mabuti **(Kwa mwanafunzi wa fani ya Uashi)** | Jozi 1 |
| 13 | Vifaa vya kutumia wakati wa chakula, na vifaa kwa matumizi binafsi kama dodoki, chanuo, brashi, mswaki, chandarua n.k. **(Kwa mwanafunzi wa bweni)** | |

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI- VETA

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WOTE

### ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO: -

**1. MAHUDHURIO:**

a. Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.15 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1.15 asubuhi wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji**.
b. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya Chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile wakati wa masomo bila ya kuruhusiwa na mwalimu wake wa darasa (Mkuu wa Sehemu).
c. Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima atoe taarifa kwa Mkuu wa chuo, Msajili au Mwalimu wake wa darasa. **Kutofanya hivyo ni kosa**.
d. Mahudhurio chini ya 85% kwa muda wote wa masomo, mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo.

**2. MAVAZI:**

**a.** Sare ya chuo ni suruali ya bluu, shati jeupe la mikono mirefu, sweta la blue, T-shirt ya chuo na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba. Sare hizo zivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. **Wakati wote shati liwe limechomekewa.**
b. Hairuhusiwi kubadilisha mshono na vipimo vya suruali iliyoshonwa hapa Chuoni. Ukifanya hivyo suruali yako itachanwa na kutakiwa kulipia nyingine au kuondolewa chuoni.
c. Ovaroli na viatu vya usalama (Safety boots) vivaliwe wakati wote wa vipindi vya kazi za mikono kwenye karakana.
d. Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au sandozi, haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.
e. Hairuhusiwi kwenda na sare ya chuo sehemu za starehe kama vile baa, sinema au sehemu zinazolingana na hizo.

**3. USAFI WA MWILI:**

a. Hairuhusiwi kuvaa heleni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.
b. Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali au mbaya kiasi cha kusumbua watu wengine
c. Kupaka rangi midomo na kucha haviruhusiwi.

d. **Nywele kwa wavulana**:
   i. Zikatwe ziwe fupi na mtindo kama PANKI na KIPARA haviruhusiwi kabisa.
   ii. Ndevu zinatakiwa kunyolewa zote. **Kufuga ndevu ni kosa**.

**e. Nywele kwa wasichana:**
   i. Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kwenda nyuma (twende kilioni)
   ii. Nywele ndefu na zenye kupakwa madawa kama vile Karl, raster na golden hair haziruhusiwi kabisa kwa kipindi chote cha mafunzo.

**4. UTUNZAJI WA MALI NA MAZINGIRA CHUONI:**

a. Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja na/au kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.
b. Ukipoteza vifaa vya chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe na ukilete ili kufidia ulichopoteza.
c. Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.
d. Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini.
e. Uongozi wa chuo hautalazimika kushughulikia wizi wa mali ya mwanafunzi yeyote ambaye hakutoa taarifa ya umiliki wa mali hiyo pindi alipofika chuoni.
f. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa balozi mzuri kwa kutunza mazingira ya chuo pamoja kuzingatia usafi binafsi wa mwili

**5. UGOMVI:**

a. Ugomvi, kupiga au kupigana na kushambulia kwa maneno ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya kisheria.
b. Kufanya jaribio la kuua au kujiua ni kosa litakalopelekea kufukuzwa chuo

**6. ULEVI:**

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo, anavuta sigara, bangi au madawa ya kulevya katika kipindi cha mafunzo adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

**7. MAPENZI:**

a. Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.
b. Mwanafunzi akiwa na mimba hataruhusiwa kuendelea na masomo.
c. Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.
d. Ubakaji na ushoga ni makosa yatakayopelekea kufukuzwa chuo Pamoja na hatua za kisheria kuchukuliwa zidi ya wahusika

**8. MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

**9. LUGHA YA MAFUNZO:**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kufanya bidii ya kujifunza kiingereza kwa namna yoyote.

**10. JINA** lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum za mahakama kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

## 11. MATUMIZI YA SIMU ZA MKONONI

Haitaruhusiwa kuonekana na simu ya mkononi darasani kwa muda wote wa vipindi. Matumizi yoyote ya simu darasani yatapelekea kunyang'anywa simu yako na kusimamishwa masomo.

## SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI

**Ili uishi na uyafurahie maisha ya bweni zingatia yafuatayo:-**

1. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo:
   - (i) Jumapili kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.
   - (ii) Jumamosi kuanzia saa 5:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.
   - (iii) Jumamosi saa 1:30 hadi 4:50 asubuhi ni usafi wa jumla mabwenini, mwalimu wa zamu na walimu walezi wa mabweni watapita kufanya ukaguzi wakati huo.
   - (iv) Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati mwingine wowote bila kibali maalum.

2. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuvaa sare ya Chuo yenye nembo ya VETA. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuvaa sare yenye nembo ya VETA atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kuishi bwenini au kufukuzwa Chuoni.

3. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kibali atasimamishwa masomo na kunyang'anywa nafasi ya kuishi bwenini.

4. Hairuhusiwi kupika chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali, ikiwa ni pamoja na kuondolewa bwenini. Pia, matumizi ya 'heater' hayaruhusiwi, adhabu yake ni kufukuzwa chuo.

5. (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wa kike kutembeleana mabwenini.
   (b) Hairuhusiwi kabisa kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa Chuo bila ruhusa au kibali.
   (c) Wanafunzi wa kutwa hawaruhusiwi kwenda mabwenini isipokuwa kwa kibali maalum.
   (d). Wanafunzi wa kutwa hawaruhusiwi kuwepo chuoni baada ya muda wa vipindi kuisha, isipokuwa kwa ruhusa maalum itakayotolewa na Mkuu wa Chuo.

6. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalumu kutoka kwa Mwalimu wa Zamu itatolewa.

7. Taa za madarasani zizimwe ifikapo saa 4:00 usiku, na mabwenini kwenye vyumba zizimwe ifikapo saa 4:30 usiku.

8. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo ni lazima kumjulisha Mwalimu wa bweni au mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.
   Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao (wanachuo) kila:-
   (a) Jumamosi kuanzia saa 6:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.

(b) Jumapili na siku za Sikukuu kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka 11:00 jioni.

9. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye viti, madawati au kuta za majengo ya Chuo.

10. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya Chuo itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo.

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNZI STADI-VETA**
**CHUO CHA UFUNDI STADI – VETA NJOMBE**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**A) MWANACHUO**

Mimi ………………………………………………………………. ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Sahihi……………………………………………… Tarehe…………………………………………

**B) MDHAMINI**

Mimi ……………………………………………………………… Simu na.............................. ambaye ni (Mahusiano)…………………………………………….... wa mtajwa hapo juu, ninayeishi (mji)……………………………………………………………… nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Sahihi ………………………………………………. Tarehe……………………………………………

**MUHIMU:**

Fomu hii irudishwe /itumwe chuoni kabla ya tarehe 13/01/2025 kwa kutumwa kwenye barua pepe ya chuo ambayo ni: **njombervtsc@veta.go.tz**

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**

The Medical Officer
Date……………..
……………………………….
……………………………….
……………………………….
……………………………….

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR (Name)**

**…………………………………………………………**

Please examine the above named candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an…………………………………………….

(i) Eyesight……………………………………………
(ii) Hearing……………………………………………
(iii) Asthma……………………………………………….
(iv) Epilepsy……………………………………………….
(v) Other serious diseases………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE:**
I have examined the above named and consider that/she is physically fit/unfit for training as above.

**Date:** …………………… Designation: …………………………..

**Signature & Official Stamp**

………………………………….